22130199

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI A: LITERATURE – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI A : LITTÉRATURE – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI A: LITERATURA – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Wednesday 8 May 2013 (morning)
Mercredi 8 mai 2013 (matin)
Miércoles 8 de mayo de 2013 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a guided literary analysis on one passage only. In your answer you must address both of the guiding questions provided.
- The maximum mark for this examination paper is *[20 marks]*.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N’ouvrez pas cette épreuve avant d’y être autorisé(e).
- Rédigez une analyse littéraire dirigée d’un seul des passages. Les deux questions d’orientation fournies doivent être traitées dans votre réponse.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d’examen est *[20 points]*.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un análisis literario guiado sobre un solo pasaje. Debe abordar las dos preguntas de orientación en su respuesta.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es *[20 puntos]*.




© International Baccalaureate Organization 2013

https://xtremepape.rs/

*Andika uchambuzi kuhusu kifungu* ***kimoja*** *kati ya hizi. Ni lazima kuzingatia maswali mawili uliyotolewa kama mwongozo kwenye jibu lako.*

**1.**

Tulikuwa darasani tukisoma somo la Kiswahili kulipozuka kioja. Mapembe, kijana mkaidi aliyechukua somo la Kiswahili aliamua kuvuka mipaka. Hakufanya zoezi la mwalimu na alipoulizwa kuelezea sababu aliota ukali wa pilipili.” Sitaki kusoma Kiswahili! Hii ni lugha ya matopasi tu na mimi sikusudii kuwa topasi! “Alijibu.”

Maneno yake yalikuwa na ncha kali. Sote tuliangua kicheko darasani kwa sababu ya ujasiri wake. Hata hivyo, tulimuona mjinga na kwa hakika alikuwa mjinga. Wenyewe tulikuwa kibindoni na faida za Kiswahili na hivyo aliyefanya uamuzi wa kijinga kama yeye hatukuwa na budi kumuacha aliwe na ujinga. Wajinga ndio waliwao. Kwa kuhofu hasira za mwalimu, Mapembe alichomoka darasani kama chui aliyekuwa mawindoni. Hatukumfuata. Tuliendelea na kipindi chetu kama kawaida huku mada ya kipindi ikibadilishwa kutoka vivumishi hadi kwenye umuhimu wa lugha ya Kiswahili maishani.

Kwa wengi wetu tulifahamu fika utamu wa lugha, tulitaja dhima hiyo hata mwalimu akashtuka. Si kufundisha, si kutunga nyimbo na michezo ya kuigiza, si kuhariri, si uhatibu, si uandishi bali tulifahamu kwamba lugha hiyo ilikuwa na umuhimu mkubwa kuunganisha jamii yetu na kutupa kitambulisho aula kama taifa tunapokuwa ughaibuni.

Aibu ya kurudi shuleni kukabiliana na mwalimu wa Kiswahili ilimkamba Mapembe koo na kuzuia safari yake ya kurudi shuleni humo. Alitafuta shule nyingine alikosomea hadi alipomaliza masomo yake ya shule ya msingi. Aliendelea na masomo yake hata akamaliza shule ya upili. Somo la pekee alilopita lilikuwa somo la hesabati japo asingeweza kwenda chuoni kwa sababu ya kufeli masomo mengine. Alilia ngoa akalaumu mfumo wa elimu lakini asingeweza kuukata kwa hivyo hakuwa na budi kuubusu.

Jumamosi moja alikuwa katika pita pita zake za kutafuta vibarua aliposhtukia akibisha ofisi ya Mwaoni. Mwaoni alikaa dawati moja naye shule yake ya kwanza na sasa alikuwa mhariri wa vitabu katika shirika moja maarufu. Mapembe alipomwona, alishusha pumzi ya matarajio. Alijua taifa lake lilikuwa na uraibu wa “umjuaye nani?” na kwa kuwa yeye alimfahamu Mwaoni aliiona kazi mikononi mwake.

“Nikusaidieje sasa?” Mwaoni aliuliza. “Kazi rafiki yangu,” Mapembe alijibu. Sijui maneno yake yaliamsha nini katika fikira za Mwaoni, nilichosikia ni kicheko kikubwa cha kejeli kikimtoka Mwaoni. Alicheka kama mwehu. Badala ya kutoa jibu aliangalia saa yake akapata ni saa tatu na robo asubuhi, wakati wa kuanza kwa kipindi cha kurunzi ya lugha kwenye radio faulu.

Kurunzi ya lugha kiliongozwa na mtangazaji mmoja maarufu Issa Mkambe. Mapembe alipoisikia sauti tu alitambua moja kwa moja kwamba yule alikuwa Mkambe, yule yule waliocheza naye kandanda shule ya kwanza. Bwana huyu alilemewa. Kilichomshtua hata zaidi ni mshahara wa nusu millioni aliouweka kibindoni Mkambe. Mapembe alilemewa. Alitamani kulia lakini machozi hayakumtoka. Mwaoni (mhariri wa Kiswahili), Mkambe (mtangazaji wa Kiswahili) Pima (mtunzi wa michezo ya kuigiza) na Zainabu (mwimbaji wa taarabu). Zilikuwa habari za kumliza Mapembe. Alilia lakini kilio chake kilikuwa cha mdharau biu hubiuka.



https://xtremepape.rs/

Bila ya kuendelea na mazungumzo zaidi, aliondoka ofisini mwa Mwaoni taratibu huko miguu yake ikiwa mizito kama nanga. Machoni alikuwa akifutafuta machozi. Kilio cha ndani sasa kilikuwa kimetoka nje. Baada ya mwezi mmoja hivi, Mapembe alirudi ofisini mwa Mwaoni. Mara hii alikuwa na uamuzi maalum. Alitaka kusaidiwa kupata kazi yoyote iwayo. Mwaoni hakumvunja moyo. Alimtuma kwenye idara ya kupakia vitabu kwenye lori. Hii ingemlipa shillingi elfu tano kila mwezi. Alipofanya kazi kwa mwezi mmoja, Mapembe alimwendea Mwaoni na ombi jipya. Aliandika ujumbe kwa karatasi na kumpa Mwaoni.

“Nisaidie. Nataka kurudi shule nikasome Kiswahili,” ujumbe ulisema.

Mwaoni alipomtazama machoni, machozi yalikuwa yakimtoka njia mbili, alikuwa katika kilio.

Kilio hicho kilikuwa awamu nzuri kwake kujifunza ukweli kuwa anayepuuza usuli wake ni adui wa hatima yake mwenyewe na mwacha kiwi hanacho na chema kimpotelee.

Joseph Mwamburi na Henry Indindi, *Kurunzi ya insha darasa la 6–8* (2011)

(a) Onyesha vile mwandishi anavyotumia mbinu ya sadfa katika kutekeleza maudhui yake. Tumia mifano mwafaka kutoka kwenye kifungu hiki.

(b) Jadili vile sifa za wahusika zinavyochangia katika kuendeleza lengo kuu la mwandishi na uonyeshe jinsi majina ya majazi yanavyofanikisha kazi ya mwandishi.



https://xtremepape.rs/

**2.**

**Kheri Upate Nambiya**

Kwa wangu alo moyoni, kiyangazi na masika
Nanena ya mtimani, bila ya kufedheheka
Pendo la tangu zamani, lipate kueleweka
Na kama nina kasoro, kheri upate nambiya.

Ni wangu moyo waliya, ukinena ya mahaba
Mahaba kanivamiya, moyo wangu kuukaba
Hadi kanilazimiya, nifichuwe langu huba
Na kama nina kasoro, kheri upate nambiya.

Sitaki uje ropoka, porojo ukazitiya
Habari sije ponyoka, waja wakatangaziya
Heshima ikanitoka, hadhi ukanishushiya
Na kama nina kasoro, kheri upate nambiya.

Hino siri ni ya weye, usimwambie mwengine
Nataka weye na miye, asiwe kati mwengine
Ndiwe unipendezaye, hakuna mja mwengine
Na kama nina kasoro, kheri upate nambiya.

Utulize wangu moyo, wahaka kuniondowa
Mawazo niliyo nayo, yanigeuza mtawa
Tiba nipa wako moyo, wala sitie madawa
Na kama nina kasoro, kheri upate nambiya.

Uza hata na wa kale, ni lini wakati upi
Vitaze vishindikile, mahaba kwa mbinu zipi
Ni lipi lijile mbele, ya mahaba nena lipi?
Na kama nina kasoro, kheri upate nambiya.

Mbona wanipa mashaka, ewe wangu wa moyoni
Na ndivyo nahangaika, huku nawe hunioni
Vichakani namulika, kajifita sikuoni
Na kama nina kasoro, kheri upate nambiya.

Mhariri wa tabiya, zako nimezihariri
Nionele zavutiya, nikazitiya muhuri
Nazo kanipendezeya, ndipo katunga shairi
Na kama nina kasoro, kheri upate nambiya.



https://xtremepape.rs/

Nitabakiya weleni, japo unikataliye
Nikangiya mashakani, punguwani nibakiye
Taingiya ukatani, raha inipungukiye
Na kama nina kasoro, kheri upate nambiya.

Nijibu pasi kusita, majibu upate tuma
Kabla mwiya kupita, raha yangu ikakoma
Nikachoshwa na kuteta, mtoni nikajitoma
Na kama nina kasoro, kheri upate nambiya.

Mwiti-O-M'Marete, *Pepo Nne: Diwani Ya Malenga Wa Mlima Meru* (2009)

(a) Onyesha mpangilio anaoutumia mwandishi katika shairi hili na uonyeshe jinsi anavyofaulu kuwaridhisha na kuwatosheleza wasomi wake.

(b) Jadili jinsi mwandishi anavyofaulu kupitisha ujumbe wa mahaba (mapenzi) huku ukitoa maoni yako kuhusu jinsi mitindo anayoitumia inavyofanikisha au kutofanikisha upitishaji wa ujumbe.



https://xtremepape.rs/